BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
[illegible]
TELEPHONE [illegible] NAIROBI KENYA

# IWE NURU

Januari, Februari, Machi 1974



## Nyumba ya Kikristo

# NYUMBA YA KIKRISTO

## YALIYOMO

JANUARI

MPANGO 1: Biblia Yafundisha Kuhusu Nyumba ya Kikristo

MPANGO 2: Mke Wa Kikristo

MPANGO 3: Kuwazoeza Watoto Wetu

MPANGO 4: Kumwabudu Mungu Katika Ibada ya Jamii

FEBRUARI

MPANGO 1: Kuwatunza Watoto

MPANGO 2: Kuwasaidia Watoto Wetu Wajitayarishe Kwa Utu Uzima

MPANGO 3: Shida Za Nyumbani. Uzinzi na Kuwa na Zaidi ya Mke Mmoja

MPANGO 4: Matatizo Ambayo Huleta Huzuni Nyumbani

MACHI

MPANGO 1: Juma La Maombi

MPANGO 2: Shida Za Nyumbani: Woga

MPANGO 3: Shida Za Nyumbani: Kuagua na Kuvaa Hirizi

MPANGO 4: Jitihada ya Upatanisho Katika Yesu Kristo

MPANGO 5: Misaada Zaidi

| Kipindi | Siku ya Kutangazwa | Wakati (Saa) |
| --- | --- | --- |
| Wazo la Usiku | Kila siku | 5:00 Usiku |
| Wazo la Siku | Kila siku | 12:00 Asubuhi |
| Ibada Katikati ya Juma | Kila Jumatano | 10:45 Jioni |
| Ibada ya Jumapili Asubuhi | Kila Jumapili | 2:30 Asubuhi |
| Ibada ya Jumapili Jioni | Kila Jumapili | 3:30 Jioni |
| Robo Saa ya Watoto | Kila Alhamisi | 10:45 Jioni |
| Our Man on the Mike (Eng.) | Kila Jumapili | 1:45 Asubuhi |
| Sunday Service (English) | Kila Jumapili | 2:00 Asubuhi |
| Epilogues | Kila Siku | 5:00 Usiku |
| Lift Up Your Hearts | Kila Siku | 1:50 Asubuhi |
| Daily Service | Kila siku | 3:15 Asubuhi |



# BIBLIA YAFUNDISHA KUHUSU NYUMBA YA KIKRISTO

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:

> Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana, Yesu, mkimshukuru Mungu kwa yeye. Wakolosai 3:17

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Mungu aliianzisha nyumba ya jamii ya Kikristo. Kuufuata mpango wa Mungu huleta shangwe na furaha. Leo tutajifunza baadhi ya mafundisho ya Biblia kuhusu jamii ya Kikristo.

Nyumba ya Kikristo ikoje? Ni nyumba ambayo wazazi na watoto ni Wakristo. Mkristo ni mtu ambaye amezitubu dhambi zake. Amemwungama Yesu kama Mwokozi wake na Bwana wa maisha yake. Amejitenga kutokana na njia ya dhambi na Shetani. Anamfuata Yesu katika maisha yake ya kila siku. Lakini inawezekana vijana wadogo wa nyumba kama hiyo hawajamkiri Yesu.

Kila kitu tufanyacho katika nyumba zetu ni lazima kifanywe katika jina la Yesu. Hivi ndivyo tuambiwavyo na kifungu chetu cha kukumbuka (Wakolosai 3:17).

## SEHEMU YA KWANZA: BABA WA NYUMBA

Mungu alimweka mwanamume kuwa kama kichwa cha Nyumba (Soma Waefeso 5:23). Mungu alimpa mwanamume madaraka mengi.

Inambidi mwanamume ampende mkewe, kama Kristo alivyolipenda kanisa. Na kumpa mke heshima (1 Petro 3:7). Mke ni msaidizi wake wala si mtumishi. Pia mume atawapenda watoto wake.

Mume atayatosheleza mahitaji ya jamii yake. (Soma 1 Timotheo 5:8.) Katika kifungu hiki twasoma kwamba mtu ambaye hawatunzi watu wa jamii yake ni mbaya zaidi kuliko mtu ambaye si mwamini.

Baba ni kiongozi wa kiroho katika nyumba. Zamani, Yoshua, kiongozi wa watu wa Kiyahudi, alichagua kumfuata Mungu. Alisema, "...Lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana." (Yoshua 24:15). Yoshua alikuwa kiongozi wa kiroho katika nyumba yake. Alichagua ya kwamba yeye na jamii yake watamtumikia Bwana.

Inambidi baba wa Kikristo amthibitishe Kristo maishani mwake. Inambidi aongoze katika ibada ya jamii. Inambidi ashirikiane na mkewe kwa kuwafundisha watoto mambo yaliyo sawa. Inambidi aende kanisani pamoja na jamii yake (Soma Waefeso 6:4).



## T A N Z A N I A

| Kipindi | Siku ya Kutangazwa | Wakati (Saa) |
|---|---|---|
| Inueni Mioyo | Kila siku | Asubuhi |
| Tumwabudu Mungu | Jumapili | 7:30 Mchana |
| Tumsifu Mungu | Jumapili | 4:30 Asubuhi |
| Kumekuchwa | Jumapili | 5:00 Usiku |
| Let Us Praise the Lord | Jumapili | 3:00 Asubuhi |
| Epilogue | Jumapili | 4:30 Usiku |

Tunamwomba nyote mweze kutusaidia katika kazi hii, kwa maombi yenu, na pia kwa kushiriki katika kutoa vipindi hivi, ili Mungu aibariki kazi hii. Pia twataka kuwapigia asante sana ninyi nyote ambao kwa wakati fulani mmetusaidia katika kutoa vipindi ama kwa nyimbo. Mungu na awabariki ninyi nyote.

----------------

Walitoa vipindi katika Sauti ya Kenya kwa kuvifanyia huko. Pia, Wabatisti walikuwa baadhi ya watu wa kwanza kutoa picha zao za sinema ili kutumiwa kwenye televisheni mnamo siku za mwanzo za televisheni humu nchini.

Baadhi ya vipindi vinavyotayarishwa na studio yetu na ambavyo mmoja aweza kusikiza ni hivi vifuatavyo:





SEHEMU YA PILI: MAMA WA NYUMBA

Kwanza Mungu alimwumba mwanamume. Kisha Mungu alimtengenezea mke yule mwanamume. Mke aliumbwa ili awe msaidizi wa mume wake. Biblia yatufundisha kwamba mke inampasa amtii mumewe, kama vile kanisa linavyomtii kusudi la Kristo (Soma Waefeso 5:22-24).

Pia, mwanamke ana kazi muhimu ya kuwazoeza watoto wake. Pamoja na mumewe, husaidia kuwafundisha kuhusu Mungu. Mara nyingi mwanamke huwa pamoja na watoto wadogo kuliko mume. Mke ana nafasi nyingi za kuwafundisha wampende Mungu na kuzijua habari zake. Mwanamke inampasa awafundishe wanawe tabia nzuri. Ni lazima asiwaruhusu kugombana au kulaani. Mwanamke inambidi kuwafundisha watoto kuheshimu. Inambidi awafundishe tabia nzuri kwa busara.

Twalipata kielelezo cha mwanamke mwaminifu katika Mithali 31:10-31. (Mwulize mwanamke awezaye kusoma vizuri avisome vifungu hivi.)

SEHEMU YA TATU: WATOTO

Mungu huwapa wazazi watoto kama baraka. Biblia yafundisha mambo mengi kuhusu watoto.

Watoto wanaamriwa waheshimu na kuwastahi wazazi wao. (Soma Waefeso 6:1-3).

Mungu huwaamrisha wazazi wawazoeze watoto wao. (Soma Mithali 22:6.) Vifungu

vingi katika kitabu cha Mithali vinawafundisha wazazi wawaadhibu watoto kwa makosa wanayotenda. Adhabu inafaa itumiwe katika kuwafundisha watoto mambo mazuri ambayo ni sawa kwao kuyafanya. Mzazi inambidi amwadhibu mtoto atendaye makosa kwa sababu anampenda mtoto yule. Wazazi inawabidi wasiwaadhibu watoto hali wakiwa na hasira.

Wazazi wanaamrishwa kuwafundisha watoto wao Neno la Mungu na sheria zake. (Soma Kumbukumbu la Torati 6:4-7.) Njia ya Mungu ni njema; afadhali ifuatwe. Kuabudu nyumbani ni njia ya Mungu; tujaribu kuifuata. Kuhudhuria kanisani bila kukosa ni njia ya Mungu; tuifuate. Wazazi wawafundishe watoto wao zaidi kwa yale mambo wanayoyafanya kuliko mambo wanayoyasema.

<u>SEHEMU YA NNE</u>: SHAHIDI WA NYUMBANI

Mwanafunzi mmoja aliitembelea jamii ya Kikristo. Yule mwanafunzi alisema kwamba hakuwa akimwamini Mungu.

Yule mama wa Kikristo alisema, "Ninataka nikuambie kuhusu Yesu. Ninataka nikusaidie umjue."

Yule mwanafunzi alijibu. "Huhitaji kuniambia kitu cho chote. Nimeshasikia habari za Yesu lakini bado sijamwamini. Sihitaji maneno yako yaniambie habari za Yesu. Ninamtazama ninyi nyote katika nyumba hii. Ninaona maana ya kumjua Kristo katika jamii yenu."





wakachaguliwa kuisimamia kazi hii ya Redio nao wangali wanaendelea hata sasa.

Studio ilimalizika kujengwa mwaka wa 1969. Vyombo vyote vilivyomo vya kuchukua sauti vilitoka Amerika. Na kwa sasa, vipindi vyote ambavyo Wabatisti hutoa kwa kutangazwa redioni, vinatengenezewa humo.

Kwa sababu kazi inaendelea kukua na kuongezeka, Bwa. na Bi. Clarence Allison pia wamejiunga ili kusaidiana na Bw. na Bi. Hooper katika kazi hii. Kadhalika tunaye msichana mmoja aliyetumwa kutoka Amerika ili kuja kusaidia kwa muda wa miaka miwili tu. Yeye ni Bi. Elain Lidholm. Pamoja na hawa, kunao wafanya kazi wenyeji watatu.

Kwa wakati huu, Baptisti Communications hutoa vipindi kama 450 na zaidi kila mwaka. Vipindi hivi hutangazwa kupitia vituo vya Sauti ya Kenya, Redio Tanzania na pia Redio Voice of the Gospel Addis Ababa, Ethiopia. Kunao mipango ya kuanza kupeleka vipindi vyetu katika kile kituo cha Far East Broadcasting Company ambacho kiko katika kisiwa cha Seychelles. Pamoja na vipindi hivi, pia nyimbo huchukuliwa na hata michezo ya kuigiza redioni. Utangazaji wa Neno lake Mungu kwa njia ya Cassettes pia umo katika mipango ya siku za usoni.

Ningependa kutaja ya kwamba, hata ingawa studio yetu haikuwa tayari mpaka mwaka wa 1969, hii si kusema ya kwamba Wabatisti hawakuwa wakitoa vipindi la.

## BAPTIST COMMUNICATIONS

Hapa nchini Kenya, vipindi vya Kikristo kwa njia ya redio vilianza kusikika mara tu baada ya vita vya pili vya Dunia, yaani baada ya mwaka wa 1945.

Hivi vipindi vilitangazwa kutoka kituo cha utangazaji cha wanajeshi wa Uingereza (British Forces Broadcasting Station) kilichokuwako hapa Kenya. Ni W kristo wachache tu ndio walihusika kwa kuvitoa vipindi hivyo. Pia hawakutumia lugha nyingi, bali lugha kama mbili tu, Kiswahili na Kiingereza.

Baadaye, wakati ule wa siku za hatari katika Kenya, yaani Mau Mau, yapata mwaka wa 1952 kuendelea mbele, ndipo tena matangazo ya Kikristo yakaongezwa kuwa mengi pia lugha mablimbali zikaanza kutumiwa.

Kazi ya Wabatisti ilianza humu nchini mnamo mwaka wa 1957/58. Na mara tu baada ya mwaka wa 1959, wakati ambapo kazi ya uchapishaji wa vitabu na vikaratasi vya shule ya Jumapili (Publications) ilipoanza, Misheni ya Kibatisti ya Mashariki ya Afrika pia ilianza kufikiria uwezeka wa kujenga studio ya kuwawezesha kutayarisha vipindi vya Kikristo kwa njia bora.

Mnamo mwaka wa 1968, kwa uwezo wake Mungu, mipango ilikamilika ili kuanza ujenzi wa studio ama kituo hicho. Naye Mmisheni mmoja na jamaa yake, wakajitayarisha kazi hiyo nao Bw. na Bi. Hooper





Yule mwanamke Mkristo na bwana yake waliomba sana. Walimwuliza Mungu awape nguvu ili waweze kutembea kwa uaminifu katika njia ya Kristo mbele ya yule mwanafunzi. Waliomba kwamba yule mwanafunzi aliyekuwa amepotea ataona vile ilivyo furaha kumjua Kristo kama Mwokozi. Walimwombea kijana yule ili aweze kumpokea Kristo pia.

Baadaye, akiwa katika mahali pengine, mwanafunzi yule alimpokea Yesu kuwa Mwokozi wake.

Nyumba zetu za Kikristo ni lazima ziwashuhudie wale ambao huja kututembelea. Ni lazima tuishi maisha ya Kikristo kila siku. Ni lazima tuzungumze na wengine kuhusu maana kuu ya Yesu kwetu. Hali tukiomba kila siku, twaweza kumwuliza Mungu kwa nguvu yake ya kushuhudia.

KIONGOZI: Mungu alitaka sote tuwe na nyumba za Kikristo. Tukiwa akina mama, twajua kwamba tuna mambo mengi ya kufanya katika nyumba zetu. Wakati mwingine huchoka sana, Wakati mwingine hatujisikii vizuri. Wakati mwingine ni vigumu kuwa watulivu na wema.

Kila mara twaweza kumwomba Mungu atupe nguvu yake. Atatujaza uwezo wake wa Roho Mtakatifu. Twaweza kumwamini Roho Mtakatifu ayatawale maisha yatu.

MAOMBI

(Kila mwanamke aweza kukiinamisha kichwa chake na kuomba hali akiwa kimya.) Fikiri kuhusu jamii yako. Fikiri vile unavyomtaka Mungu aifanye jamii yako. Mwulize afanye kazi katika maisha yako. Mwombee mume wako. Waombee watoto wako.

Tuombe kwamba watu wengi wasikie habari za Yesu Kristo kisha wamwamini kwa njia ya mahubiri ya radio. Tuwaombee watu wale wanaohubiri na kusema habari za Kristo katika radio. Tuiombea wafanyi kazi wa Baptist Communications.





MWISHO:

Tazama tena orodha ya madokezo. Chagueni dokezo ambalo kundi lenu laweza kufanya. Kanisa nzima pamoja na Jumuia Ndogo zinahitaji kupanga mipango kuhusu mambo mengi ya haya, lakini hata wanawake wataweza kufanya mengi. Chagueni mojawapo ya mambo kutoka katika orodha ya SEHEMU YA NNE na SEHEMU YA TANO ambayo kundi lenu laweza kufanya katika Juma hili.

MAOMBI:

Tuombe kwamba vijitabu (tracts) vinavyotolewa vitasomwa na watu wengi. Tuombe kwamba wachungaji wa Kibatisti pamoja na washiriki wa Kibatisti watakuwa waaminifu katika kushuhudia kwa njia ya kuwapa watu vijitabu.

mbalimbali wanakaribishwa kuhudhuria. Njia nyingine ni ya kuwa na chakula cha "Agape" katika jengo la kanisa. Watu wa Agano Jipya walikuwa wakifanya jambo hili. Walikuwa wakiwapa watu wote chakula; tajiri au maskini, watumwa au wasiyo watumwa wa kutoka katika makabila na mataifa yote. Kila mtu alikuwa akileta sehemu ya chakula. Walikula pamoja wakishiriki kile chakula kilicholetwa na watu wote. Walifanya hivyo bila dhuluma. Waliongea juu ya upendo wa Mungu na juu ya mambo ya Kiroho. Pendo la Mungu katika lugha ya Kiyunani huitwa "Agape" kwa hiyo walikiita chakula hicho kuwa ni cha "Agape" au karamu ya upendo.

SEHEMU YA TANO: MAZUNGUMZO ZAIDI

1. Kutekeleza matendo ya upendo kwa watu wasiyo na bahati au riziki yao katika jamii.

2. Kuwa na mikutano kwenu nyumbani ya kujifunza Biblia na kuomba.

3. Kujifunza majina ya watu wote wanaoishi karibu nanyi, hata majina ya watu wa makabila na mataifa mengine. Mwe tayari kusaidia iwapo wanazo shida.

4. Kutumia kila mwenye kuamini kuutumia uwezo wake katika kushuhudi na kurudisha uhusiano uliovunjika.

5. Kuomba na kutoa matoleo kwa ajili ya kueneza Injili.





## MKE WA KIKRISTO

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:

> Nayaweza mambo yote katika yeye (Kristo) anitiaye nguvu.
> Wafilipi 4:13

Wimbo
ita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Mpango wa Mungu kwa jamii huleta furaha. Leo tutajifunza vile Biblia itufundishavyo kuhusu mke wa nyumbani. Inatubidi tujifunze mpango huu kwa makini. Inatubidi tusikilize kwa makini vile Mungu atufundishavyo. Na tuombe ili Mungu azungumze nasi leo.

SEHEMU YA KWANZA:

Soma (Waefeso 5:22-24.) Maandiko haya yanatuambia kwamba bwana ni kichwa cha nyumba na mkewe. Mungu huzungumza na me na humwambia ampende mkewe. Huu ni upendo mkuu. Ni kama ule upendo wa Kristo kwa kanisa. Mungu azungumza na mwanamke na anamwambia kwamba awe mtiifu kwa mumewe. Mungu alimpangia mume awe kichwa cha nyumba nzima. Mke aliumbwa awe msaidizi wa mambo yote.

Mke wa Kikristo inambidi ampende mume wake bila kizuizi na amwonyeshe mume wake upendo. Inambidi asimlaumu mumewe na kumkasirisha. Inambidi ayafurahie mambo ambayo yanamfurahisha mumewe.

SEHEMU YA PILI:

(Soma 1 Timotheo 3:11.) Mwanamke inampasa awe mtulivu na mwaminifu. Inambidi awe mwema kwa wengine.

Mama wa Kikristo hatampazia sauti au kumkemea mumewe au watoto wake. Hatakasirika upesi. (Soma Mithali 15:1).

Mke wa Kikristo atakuwa mwaminifu kwa mume wake. Hata kama ni lazima awe mbali na mumewe kwa muda mrefu, atabaki mwaminifu.

(Soma Waefeso 5:33.) Mwanamke inambidi amheshimu mume wake. Mke wa Kikristo hatawaambia marafiki wake wa nje kuhusu mambo mabaya ya mumewe. Inamlazimu amwonyeshe mumewe upendo kwa mambo yote.

SEHEMU YA TATU:

Mke wa Kikristo hujishughulisha na mahitaji ya jamii yake. (Soma Mithali 31:27.) Kazi muhimu sana ya mke ni ile ya nyumbani. Wakati mwingine wanawake ni lazima wafanye kazi mbali na nyumbani kwao ili wajipatie fedha. Walakini, inawalazimu wafanye kazi kwa bidii kuhakikisha ya kwamba jamii yake yatunzwa. Ni vigumu kufanya kazi mbali na nyumbani na





Hii siyo jitihada tu. Siyo mfululizo wa mikutano. Bali ni njia ya maisha. Ni njia ya maisha ya mwenye kuamini kuwaambia wengine juu ya pendo la ukombozi wa Mungu.

Katika kila nchi Jumuia Kuu ya Wabatisti hukaza mambo fulani yaliyo ya maana. Jambo moja la mkazo ndilo la kufundisha maisha ya kiroho. Mkazo katika sehemu nyingine huwa ni mfululizo wa mikutano ya injilisti. Mkazo wa tatu ndiyo huo wa kuibadilisha chuki na dhuluma na badala yake kuwe na upendo na undugu.

SEHEMU YA NNE: MADOKEZO KWA AJILI YA MAKANISA

1. Kuukaza upendo wa Kikristo kwa kila jamaa walioko kanisani. (Kusomea nyumbani 1 Yohana 1).

2. Kumwongoza kila mwenye kuamini kujazwa na Roho Mtakatifu. "Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho..." (Waefeso 5:18).

3. Tayarisha kila mwenye kuamini awe tayari kushuhudia.

4. Kupanga jitihada za uinjilisti katika miji mikubwa na katika Jumuia Ndogo.

5. Kutoa nafasi za kushinda dhuluma na woga. Labda jambo hili linaweza kutimizwa kwa njia ya kuwa na ushirika ndani ya nyumba, mahali ambapo watu wa makabila

Mojawapo ya uadui huo ni ule wa mwanadamu kumwasi Mungu. Hata kama mwanadamu anajua kuwa yeye ni Mungu, anakataa kumwabudu na hana shukrani. Mwanadamu anajua kuwa yeye ni mkosaji. Kwa sababu amekosa na hataki kuyatazama makosa ya roho yake, anamkasirikia Mungu. Anahitaji upatanisho.

Hata ikiwa mwanadamu hafai, Mungu ameahidi kumkomboa na kupatanisha nafsi yake na mwanadamu. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake." (2 Wakorintho 5:19).

Mungu ametupa sisi tuliokombolewa ujumbe wa upatanisho. "Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho---" (2 Wakorintho 5:18).

Ametuamuru kuwaambia wengine vile wawezavyo kupatanishwa na Mungu. "Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu" (2 Wakorintho 5:20). Tunafanya hivyo siyo kwa maana ametuamuru, bali ni kwa sababu pendo la Mungu linatuhimiza kuishiriki neema yake.

SEHEMU YA TATU: JITIHADA YA UPATANISHO KWA ULIMWENGU

Kunazo Jumuiya Kuu 94 za Wabatisti kutoka katika nchi 83 ambazo zimepiga kura kushika sehemu katika Jitihada ya Upatanisho kwa Ulimwengu katika Kristo.





pia kutunza jamii vizuri. Hata hivyo kutunza jamii ni wajibu mkuu wa mwanamke wa Kikristo.

Mke wa Kikristo inambidi aifanye nyumba yake pawe mahali pa furaha. Hata ikiwa ni maskini, anaweza kuiweka nyumba yake safi na nadhifu. Hali kadhalika, anaweza kujiweka yeye mwenyewe safi na pia watoto wake.

Ni muhimu kuwatunza vizuri watu wa jamii katika siku za mikutano ya kanisa. Mke yambidi afanye wakati wake kwa makini ili jamii isione kutotunzwa.

SEHEMU YA NNE:

Mke wa Kikristo inambidi afanyeje kwa mumewe ambaye si Mkristo? Biblia yatuambia kuwa **asimwache** bwana wake. (Soma 1 Wakorintho 7:13.) Inamlazimu afanye iwezekanavyo ili amwongoze kumkiri Kristo. Inamlazimu amshuhudie kwa maisha yake mwenyewe ya Kikristo. Aweza kumwambia mumewe kuhusu upendo wa Kristo. Aweza kueleza jinsi ya kuokolewa. Mume akikataa kusikiliza, asimlazimishe. Aweza kungojea na kuomba.

Mke wa Mkristo hawezi kumwokoa mumewe. Mungu pekee ndiye awezaye kufanya hivyo. Roho Mtakatifu huleta hukumu ya dhambi. Kila mtu ni lazima akate shauri kumpokea Kristo kwa ajili yake mwenyewe. Kwa hivyo mke ni lazima amwombee sana mumewe.

Wanawake wawili walikuwa wenye furaha sana wakati wa ibada ya ubatizo. Waume wao walikuwa baadhi ya wale waliokuwa wakibatizwa siku ile. Wanawake hawa walikuwa Wakristo kwa muda mrefu. Kwa miaka mingi walikuwa wamewaombea waume wao kwa uaminifu.

Mmoja wa wale waume alisema, "Nimemwona Kristo nyumbani mwangu. Mke wangu amenionyesha Kristo. Amekuwa mwaminifu katika maisha yake. Nimeona vile Kristo alivyoyageuza maisha yake. Nilijaribu kumkataa Kristo. Nilitaka kuishi katika maisha yangu ya zamani. Nilitakakunywa pombe na kucheza karata na marafiki wangu. Lakini moyoni mwangu nilijua kwamba haya yalikuwa makosa. Nilijua kwamba mke wangu alitembea katika njia nzuri. Sasa mimi pia nimeipata njia katika Kristo."

SEHEMU YA TANO:

Mwanamke wa Kikristo, Bi. Moyo aliolewa na mume ambaye hakuwa Mkristo. Mumewe alimwambia, "Nitengenezee pombe ili ninywe pamoja na marafiki."

Moyo wa Bi. Moyo uliumia sana. Alitulizа akaomba ya kwamba Mungu amwimarishe. Alisema, "Vizuri sana, Bw. Moyo, nitafanya kama unavyoniambia."

Hali akiwa anafanya kazi ya kutengeneza pombe, Bi. Moyo alimwomba Mungu kumsaidia bwana wake. Alisema, "Mwenyezi Mungu, nitaendelea kumwombea bwana yangu. Nitakutegemea kunisaidia ili niyaheshimu





SEHEMU YA KWANZA: UPATANISHO WA BABA NA MWANA

Lazaro Malunga wa kutoka nchi ya Zambia alimweleza mchungaji mwenzake maana ya "Upatanisho" kwa njia ya kumkumbusha juu ya desturi za watu wao.

Wakati mwingine baba na mwana hubishana mpaka wao hukata shauri kwamba watavunja uhusiano wao mbele ya watu wote. Moto wa ishara ya hasira zao huwashwa kati yao. Baba na mwana huivuta kamba kila mmoja akielekea upande mwingine.

Inambidi mtu mwingine aikate ile kamba au aichome vipande viwili. Kwa njia hii wanatangaza wazi kuwa wameuvunja uhusiano wao na hakuna ukoo kati yao tena.

Baadaye, inawezekana watapenda kusamehe au kusamehewa. Tena hutangaza wazi mbele ya watu kuwa uhusiano wao umerudishwa. Halafu mtoto huwashwa. Baba na mwana wanasimama mmoja upande huu na mwingine upande ule, wakiishika kamba. Wakati mmoja wao anapoivuta kamba mwingine humwaga chumvi juu ya moto ili kuuzima mwali wa moto. Baba na mwana wamepatanishwa tena. Badala ya kuwa na hasira huwa na upendo wa ushirika.

SEHEMU YA PILI: MIOTO YA UADUI

Ulimwenguni siku hizi kunayo mioto mingi ya uadui.

## JITIHADA YA UPATANISHO KATIKA YESU KRISTO

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:

Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu.
2 Wakorintho 5:2 )

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Pengine umeisha sikia habari za "Umisheni wa Upatanisho Ulimwenguni Ndani ya Yesu Kristo." Wajumbe wa Makanisa ya Kibatisti kutoka katika sehemu zetu za ulimwengu ambao walihudhuria mkutano wa Mwungano wa Wabatisti wa Ulimwengu katika Tokyo mnamo mwaka wa 1970 walikubaliana kuwa wakashirikiana katika jitihada hii. Mtu mmoja katika nchi yako alikuwapo wakati jambo hili lilipopitishwa. Anyingisye Mwasandube wa Tanzania na John Kariuki ) Kenya walikuwako. Leo tutatafuta kujua maana ya upatanisho na hata kufikiria njia ambazo twaweza kusaidia katika jitihada hii.





mapenzi yako kwa maisha yangu."

Wakati alipokuwa akiitengeneza pombe, Bi. Moyo alikuwa mwangalifu ili asiionje hata kidogo. Hakunywa hata tone moja la pombe. Bali aliendelea kuomba, akimweka mumewe pamoja na wale wageni mbele ya Mungu.

Uwezo wa Mungu ulionekana. Wanaume wawili wa Kikristo walikuja kuwatembelea nyumbani kwao. Walikuwa wanyenyekevu na wenye kupenda marafiki. Waliwashuhudia Bw. Moyo na wageni wake kuhusu upendo wa Kristo.

Bi. Moyo aliendelea kuomba. Kisha Bw. Moyo na mmoja wa wale marafiki zake walimpokea Kristo siku ile ile.

Leo, Bw. Moyo ameyapata maisha mapya katika Kristo. Yeye sasa ni shemasi kanisani mwake. Ana imani kuu kwa mkewe. Bi. Moyo anafuraha ya ajabu. (Soma Mithali 31:11.)

KIONGOZI:

Tukiwa wanawake wa Kikristo, twajua kwamba ni lazima Kristo awe wa kwanza maishani mwetu. Tukiweza kuwatii waume zetu, inatubidi tufanye hivyo. Walakini, ikiwa asiyekuwa Mkristo akimwamuru mkewe aache kumwamini Kristo, hawezi kumtii. Ikiwa alimwamuru kuacha kuomba na kusoma Biblia, hataweza kumtii. Ikiwa mumewe alimtaka aibe au kuivunja sheria ya Mungu, hataweza kumtii. Ni lazima tuombe na

kuyatafuta mapenzi ya Mungu kwanza. Atatupa nguvu yake. (Soma tena kifungu cha kukumbuka kwa siku ya leo.)

MAOMBI:

Omba ya kwamba sisi Wakristo tuishi ili wengine waweze kumwona Kristo ndani yetu. Natuwaombee waume zetu na watoto.

Tuwaombee waalimu wa shule ya Jumapili wa makanisa yetu. Tuombe ili walifundishe Neno la Mungu kwa njia ifaayo. Waombee watoto wanaohudhuria ili waweze kujifunza juu ya pendo la Yesu. Omba kwamba watu wazima na watoto wawe na moyo wa kuhudhuria shule ya jumapili.





MAOMBI:

Waombee wahamiaji watoro wa siasa wanaoishi katika Kenya na Tanzania. Wengi wa hao wahamiaji walilazimishwa kutoka nchi zao kwa sababu ya siasa au mateso. Wengi wao walizipoteza mali zao zote walipotoroka. Tumwombe Mungu ili awasaidie katika haja zao. Tuombe ili tupatikane nafasi ya kuwashuhudia.

SEHEMU YA TANO:

Mama mwingine wa Kikristo alikuwa na mtoto wa kupendeza. Naye mtoto alipatwa na ugonjwa mbaya. Madaktari walifanya kazi kwa bidii na hata kumwombea. Lakini mtoto alikufa.

Pia mwanamke huyo alikuwa na ushuhuda wa ajabu. Alikuwa na huzuni, lakini aliipata amani yake katika Mungu. Aliwaambia marafiki zake kwamba Mungu alimfariji moyoni mwake. Alisema, "Sielewi, naweza tu kumshukuru Mungu kwamba tulikuwa na mtoto wetu kwa muda wa miaka mitatu. Tulimpenda huyo mtoto sana. Siku moja tutakuwa na mtoto wetu mbinguni. Mungu hunifariji nikiwa katika huzuni."

Kifungu chetu cha leo cha kukumbuka kinatwambia kwamba Mungu hutufariji. Katika huzuni zetu, twajifunza kuhusu faraja ya Mungu. Twajifunza jinsi ya kuwaambia wengine kuwa Mungu aweza Kuwafariji.

KIONGOZI:

Na tuombe sasa ili tupewe uwezo wake Mungu wa kushinda woga. Natuombe ili Mungu atupe uwezo wake kwa kuikataa dhambi ya kujiagua au kwa kutumia hirizi. Tumwulize Mungu atupatie imani ya kweli iliyoko ndani yake. Ikiwa unao woga mwingi kuhusu mambo haya katika moyo wako, mwulize Mungu akuondolee.





KUWAZOEZA WATOTO WETU

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:

Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.
Mithali 22:6

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Leo tutajifunza kuhusu baadhi ya wajibu wetu kwa watoto wetu. Mzee mmoja ambaye ni muhubiri alikuwa akitembelea mji fulani. Kulikuwa na shida nyingi kwa sababu ya mataifa ya kuabudu kwa pepo. Mmoja wa watu waliokuwako alimwuliza yule mzee ikiwa amekuwa akiogopa pepo au machawi.

Yule mzee wa Kikristo alisema, "Mama yangu alikuwa Mkristo wa ajabu. Alinifundisha tu habari za Yesu na upendo wake. Nilikua nikiwa ninampenda Yesu. Sikujua woga wa wachawi na pepo. Sikuyafahamu mambo hayo kabisa!"

Siku moja, watoto wetu watakuwa wazima wa kiume na kike. Watasema walijifunza nini katika nyumba zetu? Watasemaje kuhusu sisi? Je! Twaishi maisha ya Kikristo mbele ya watoto wetu? Je! twawafundisha kuhusu Yesu? Watoto hujifunza

kutokana na vile watuonavyo tukifanya. Hujifunza kutokana na yale watusikiayo tukiyasema. Ni jambo gani ambalo wanajifunza kutoka kwetu?

SEHEMU YA KWANZA:

Tukiwa akina mama, tuna wajibu mkubwa kwa watoto wetu. Tutajifunza kuhusu baadhi ya mambo haya katika mpango mwingine. Leo tutajifunza kuhusu wajibu wetu mkuu zaidi tukiwa akina mama wa Kikristo. Watoto wetu wana mahitaji mengi. Lakini hitaji lao kuu ni kumfahamu Yesu kama Mwokozi. Kwa kuwafundisha kuhusu Yesu na upendo wake ni wajibu wetu mkuu zaidi kwao!

Twawafundishaje watoto wetu kuhusu Mungu na Mwanawe, Yesu Kristo? Twaweza kufundisha vizuri kwa vile tufanavyo na vile tunavyoishi.

Ni jambo gani ambalo watoto wetu wanaliona ndani yetu? Kila siku tuna kazi nyingi ya kufanya. Ndiyo, tuna kazi nyingi. Hata hivyo, tukitaka nguvu ya Mungu kwa maisha ya kila siku, ni lazima tutumie muda wa dakika fulani pamoja naye kila siku. Twahitaji kulisoma Neno lake ambalo ni Biblia tukimwomba azungumze na mioyo yetu. Twahitaji kuomba, tukimwuliza atupe uongozi wake kwa siku nzima. Yeye husikia na kutujibu. Ni lazima tupate wakati kila siku wa kuisoma Biblia na kuomba.





wetu ana nguvu zaidi kuliko hirizi. Siamini hirizi kuwa zina nguvu ya kuokoa au kuponya. Ninauamini uweza wa Mungu."

Mama mmoja alimleta mtoto wake katika Kliniki iitwayo "Kliniki ya watoto." Alijifunza kuhusu upendo wa Mungu kwa watoto wote wadogo. Alijifunza jinsi ya kumtunza mtoto wake. Alijifunza kuhusu sindano ambazo za kukinga magonjwa mengine. Alijifunza jinsi ya kumlisha mtoto wake vyakula vizuri. Alijifunza kwamba Mungu anao uweza. Mungu anaweza kuushinda uoga.

Alimwangalia mtoto wake. Kwenye shindo ya mtoto kulikuwa na hirizi. Kwenye kiuno pia kulikuwa na hirizi. Aliaibika. Alijua kwamba hakuwa akimwamini Mungu kwa ukamilifu. Sehemu ya imani yake ilikuwa kwa zile hirizi.

Alimwomba mwuguzi mikasi. Alizikata hirizi na kuzitupa. Nyanyaye mtoto aliudhika sana. Lakini yule mama mtoto alisema, "Nimejifunza mambo mengi ya kufanya kumsaidia mtoto wangu. Ninajifunza jinsi ya kumlisha mtoto wangu kwa njia bora ili mwili wake ukue ukiwa na nguvu. Nitayafanya mambo haya. Nitamwamini Mungu wala iyo hirizi."

Mama huyo alimlisha mtoto wake vizuri. Alimpeleka Kliniki ili akapigwe sindano. Mtoto alikua akiwa mwenye nguvu na afya. Naye nyanyaye mtoto walifurahi. Mama ya mtoto yule alikuwa na ushuhuda mzuri.

maji mengi kutoka mwilini mwake. Utosi huingia ndani kwa sababu ya upungufu wa maji mwilini. Hii ni dalili mbaya ya ugonjwa. Lakini kuingia ndani kwa ule utosi si jambo linalosababisha ugonjwa. Kuisugua dawa kwenye utosi hakuwezi kusaidia. Mtoto anahitaji kupelekwa kwa daktari. Daktari atampiga mtoto sindano kwenye mshipa. Ataiweka dawa ya maji kwenye mishipa ya mtoto. Jambo hili litasaidia kuyarudisha maji ambayo yamepotezwa kwa kutapika na kuhara. Daktari atampa dawa ya kuponya kutapika na pia kuhara. Ikiwa matibabu yatamsaidia mtoto, utosi utarudia hali yake ya kawaida.

Twajua kwamba madaktari na dawa peke yake haziwezi kuponya mgonjwa siku zote. Hii ni kweli kabisa ikiwa wazazi wanangojea kwa muda mrefu kabla ya kwenda kwa daktari baada ya mtoto kuwa mgonjwa. Ni lazima tufanye tuwezavyo. Ni lazima tumpeleke mtoto kwa daktari. Ni lazima tuombe. Kisha ni lazima tumtumainie Mungu wala siyo kuzitumainia hirizi.

SEHEMU YA NNE:

Mama mmoja alisema, "Sitaki mtoto wangu avae hirizi. Siamini hirizi. Lakini nyanyaye mtoto alimvika mjukuu wake hirizi. Ninaogopa kuzifungua. Ninaogopa nitaletewa shida na nyanyaye mtoto."

Je, mama wa Kikristo aweza kuuonyesha ukweli wa Mungu na imani yake katika Mungu? Je, aweza Kusema, "La, mama, mimi ni Mkristo. Nakwambia ya kwamba Mungu





SEHEMU YA PILI:

Bi. John alikuwa mama mzuri. Alifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watoto wake. Aliiweka nyumba yake safi na nadhifu. Watoto walikuwa safi na nadhifu. Alitayarisha chakula kizuri kwa watoto wake.

Bi. John alikuwa mama wa Kikristo. Aliwafundisha watoto wake habari za Yesu. Alienda nao kanisani kwa ibada. Lakini hata hivyo hakuwa na furaha kabisa katika Bwana. Alifikiri kwamba alikuwa na kazi nyingi hata hakuweza kuisoma Biblia yake na kuomba peke yake kila siku.

Kulikuwa na mkutano wa ufufuo katika kanisa. Bi. John alimsikiliza muhubiri akieleza kuhusu umuhimu wa kukua kiroho. Alijua ya kwamba ni lazima ale chakula kinachofaa kwa kukua kiroho. Ni lazima aisome Biblia kila siku na kuomba daima.

Bi. John aliomba kwamba Mungu ampe nguvu yake. Sasa, kila asubuhi anajitenga kuomba. Hulisoma Neno la Mungu na kumwuliza Mungu azungumze na moyo wake. Humwomba Mungu ayaongoze mafikira yake kila siku. Humwombea mumewe na watoto. Wakati wa Achana anapopata shida, humwuliza Mungu amwongoze. Mungu akisema na moyo wake, yeye humtii. Kuna amani na furaha katika maisha ya mwanawe yule. Kwa sababu yu mwenye furaha, nyumba yake ni yenye furaha kuliko ilivyokuwa zamani. Watoto wake wanafurahi pia.

SEHEMU YA TATU:

Watoto waweza kufundishwa kuhusu Mungu hali wakiwa bado ni wadogo sana. Mtoto mdogo akichukua ua zuri kwa mara ya kwanza mkononi mwake, mama aweza kusema, "Mungu ni mzuri. Mungu aliyatengeneza maua mazuri. Mungu alitengeneza kila kitu."

Wakati mama akimwambia mwanawe, "Tw kupenda" pia aweza kusema, "Mungu akupenda pia."

Watoto wadogo hupenda kuimba. Mama aweza kuwafundisha nyimbo fupi kuhusu Yesu. Watoto watajifunza kutokana na nyimbo ambazo mama yao ataziimba.

(Waambie njia ambazo wewe huwafundisha watoto wako wampende Mungu. Waulize wanawake wazungumze kuhusu njia ambazo huwafundisha watoto wao wadogo kumpenda Mungu.)

SEHEMU YA NNE:

Watoto wetu hujifunza kuhusu Mungu wakati tunapoomba sote katika nyumba zetu. Watoto wa Bi. Moyo wanajifunza. Rudo ana umri wa miaka minne. Hupenda kuomba kwa kuimba wimbo kabla ya kula. Mtoto Ruka ana umri wa miaka miwili tu. Amefunzwa kusema, "Asante sana, Yesu," baada ya dada yake Rudo kuimba. Watoto hawa wanajua ya kwamba Mungu ndiye mpaji wa mambo mazuri.





kujua ni wakati gani ambao ni kusudi la Mungu sisi au wale tuwapendao wafe. Tunapoomba twajiweka nafsi zetu na jamii zetu mikononi Mwake.

Tunapokuwa wagonjwa twawaendea madaktari wazuri ili tupate misaada. Pia twamwomba Mungu aibariki kazi ya madaktari. Kisha ni lazima tumwamini Mungu atutimizie yale ambayo ni mazuri kwetu.

SEHEMU YA TATU:

Wanawake wengi huwavalisha watoto wao hirizi. Hata wanawake wengine walio Wakristo hizitumia hirizi.

Wakati mwingine wanawake huzitumia hirizi kwa kuzuia kuhara. Hirizi zilizoko nje ya mwili haziwezi kuuponya ugonjwa ulioko ndani ya mtoto. Dawa ya kuponya kuhara inahitajika.

Wanawake wengine walio wazazi huwa na wasiwasi sana kuhusu utosi wa mtoto mchanga. (Utosi ni sehemu ya katikati ya kichwa). Wao huzitumia hirizi kwa kuulinda utosi na pia kuhakikisha kwamba itafungwa sawa. Hufikiria kwamba mabadiliko katika utosi wa mtoto huleta magonjwa mengi ya mtoto. Hii si kweli. Magonjwa ambayo mtoto aweza kuyapata yaweza kusababisha mabadiliko ya utosi. Magonjwa haya ni lazima yatibiwe kwa uangalifu. Halafu utosi utakuwa salama.

Mtoto akiambukizwa hupatwa na kuhara na kutapika kubaya sana. Naye huyapoteza

SEHEMU YA PILI:

Siku hizi watu wengi hawaendi kwa wachawi. Wanafikiria kuwa hizi ni njia za kale, lakini huwaendea wapiga ramli wa siku hizi ili kutafuta kile kitakachotukia wakati ujapo. Wapiga ramli hawa huvaa nguo za siku hizi, lakini hawatofautiani na wachawi wa kikale. Wao hujifanya kuwa wanaweza kutabiri. Wao hulipwa pesa kwa kushauriana na watu. Wale wanaowaendea ili washauriwe nao huwaamini. Watu kama hao hawamwamini Mungu kabisa. Mkristo huzipeleka haja zake kwa Mungu kwa njia ya maombi. Huutafuta msaada wa shida zake kutoka katika Neno la Mungu. Wale ambao huwaendea wapiga ramli huzitumia pesa ambazo zingewasaidia jamaa zao katika kuyatafuta mashauri ambayo hayatoki kwake Mungu.

Inawapasa Wakristo wamtumainie Mungu peke yake kama mzaidizi wao mkuu. (Soma Mitahli 3:5,6). Hawapaswi kujishughulisha na uaguzi.

Biblia hutuambia kuwa uaguzi ni chukizo kubwa mbele za Mungu. (Soma Kumbukumbu la Torati:18:10-12). Haimpasi Mkristo kujishughulisha na dhambi kama hiyo. Tur iweka imani na tumaini letu kwa Mungu peke yake.

Mungu anao uwezo wa kuponya. Tukiwa Wakristo twaweza kumwomba ili tupate kuponywa. Tunamwomba Mungu kwamba mapenzi yake yatendeke. Huenda Mungu hatamponya mtu fulani ni lazima mtu afe. Hatuwezi





Mmoja wa watoto hawa alikuwa mgonjwa. Mama yake alimpeleka hospitalini kwa kupata matibabu. Alimsikia daktari akimwombea ili apate kupona. Nyumbani mama yake na Baba yake waliomba pamoja. Walimshukuru Mungu kwa yule daktari na ile dawa. Walimwuliza Mungu awaponye mtoto wao. Mtoto yule alipopata nafuu tena, walimshukuru Mungu pamoja. Mtoto huyu anajifunza zaidi kuhusu upendo wa Mungu.

Watoto wetu hujifunza kuhusu kanisa la Mungu wakati tuendapo nao kwa Shule ya Jumapili au ibada. Hujifunza kuhusu furaha ya kutumikia wakati wanapowaona wazazi wao wakiwafundisha katika Shule ya Jumapili au wakiwa katika makundi ya vijana.

Ni muhimu kwa vijana kuanza kwenda kwa Shule ya Jumapili hali wakiwa bado ni wadogo sana. Ni muhimu kwetu kuwafundisha kuhusu Mungu tangu ni wadogo. Ni jambo gani ambalo unawafundisha watoto wako kuhusu Mungu?

KIONGOZI:

Kifungu chetu cha Biblia cha leo ni ahadi yetu. (Waombe wanawake kusema kifungu cha kukumbuka). Twaweza kuishika ahadi hii kutoka kwa Mungu. Alisema kwamba ni lazima tu wafunze watoto wetu katika njia ambazo zinawapasa wazifuate. Ni lazima tuanze kuwaongoza katika kuwazoeza njia za Mungu hali wakiwa bado ni wadogo sana. Tukifanya hivyo, Mungu anaahidi hawataiacha njia yake wakati wakiwa wazee. Wakiwa wanakua, wanaweza kuiacha njia ya

Mungu kwa muda. Lakini ikiwa kwa kweli tumewazoeza katika njia ya Mungu, watairudia. Hii ni ahadi ya ajabu. Biblia yetu yatuambia kwamba Mungu huitekeleza ahadi yake kwetu.

MAOMBI:

Waombeeni watoto wenu. Ombeni kwamba Mungu awaongoze mwe na uwezo wa kuwazoeza katika njia ambayo inawapasa kuifuata. Mshukuru Mungu kwa ahadi zake.

Waombee watu walioko katika eneo zenye njaa za Afrika ya Magharibi. Sasa mvua imeisha nyesha. lakini haiwezi kuyaleta mavuno kwa maana ilinyesha kama imechelewa. Omba ili chakula kiwafikie watu wenye njaa. Utoe shukurani kwa sababu Wabatisti wa ulimwengu wote waliweza kusaidia.





SEHEMU YA KWANZA:

Mtu na mkewe waliishi katika kijiji fulani. Walikuwa na watoto wawili. Yule mtoto wa kwanza alikuwa mgonjwa sana. Walijaribu kumpa madawa ya kienyeji, lakini yule mtoto alifariki.

Baba na mama wa yule mtoto walimwendea mchawi wa kienyeji kwa madhumuni ya kutafuta kitu kilichosababisha kifo cha mtoto wao wa kwanza.

Yule mchawi alipiga ramli. Aliwaambia wazazi kwamba mtoto wao alikuwa ameuawa na mama mzazi wa baba wa mtoto aliyekufa. Wale wazazi waliyasikiliza maneno ya yule mchawi. Walirudi kwao nyumbani wakiwa kimya.

Kulikuwa na mabishano mengi kati yao kwa yale mchawi aliyoyasema. Mama yake mtoto aliyekufa aliogopa. Alitoroka kutoka nyumbani akamchukua yule mtoto wa pili. Aliondoka akaenda kutafuta mahali pa kuishi katika jimbo lingine. Mambo haya yote yalimletea mwanamke, mumewe na mtoto wao shida nyingi.

Kuagua husababisha shida nyingi kwa jamii. Jambo hili laweza kuharibu nyumba iliyo na furaha. Wakati mwingine kuagua humwingiza mtu kumwua mwingine. Hii ni dhambi iiletayo huzuni kwa kila mtu.

## SHIDA ZA NYUMBANI: KUAGUA NA KUVAA HIRIZI

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:

> Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu faraja yetu atufarijiaye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki.
>
> 2 Wakorintho 1:3,4

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Leo tutajifunza kuhusu mambo mawili zaidi ambayo yaweza kuleta shida katika nyumba ya Mkristo.

Tumeisha zungumza kuhusu woga na uchawi. Tumezungumza kuhusu shida ambayo uchawi waweza kuleta. Leo tutazungumza kuhusu sehemu nyingine ya uchawi. Yaani kuagua. Wakristo wengi siku hizi hutenda dhambi kwa njia hii.

Katika Hesabu 32:23, twasoma hivi, "...Ninyi mmefanya **dhambi** mbele za Bwana, nanyi jueni ya kwamba hiyo dhambi yenu itawapata hapana budi."





## KUMWABUDU MUNGU KATIKA IBADA YA NYUMBANI

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:

> Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.
>
> Kumbukumbu la Torati 6:5

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Nyumba ya Kikristo inamweka Kristo katika nafasi ya kwanza. Je! twawezaje kumweka Kristo katika nafasi ya kwanza ya nyumba zetu? Njia moja muhimu ni kuwa na wakati mfupi kila siku kwa jamii kulisoma Neno la Mungu na kumwomba.

Leo tutajifunza kuhusu kuabudu kwa jamii.

SEHEMU YA KWANZA:

) Yesu apenda kuwa nyumbani mwetu. Ni lazima tumkaribishe ikiwa twataka aingie (Soma Ufunuo wa Yohana 3:20).

Wakati Wakristo wawili wakioana, inawabidi waendelee kuomba pamoja kila siku. Bi. William Tolbert ni mwanamke wa kwanza wa Liberia. Mumewe ni rais wa nchi yake. Mwanamke huyo ana ushuhuda wa

ajabu kuhusu nyumba yao.

Bi. Tolbert alisema ya kwamba walikuwa na arusi ya kufana sana. Wageni waliokuwa wamealikwa walipoondoka, walibaki wao wawili. Kisha walipiga magoti pamoja kwa maombi. Walimshukuru Mungu kwa siku yao ya arusi. Walimwuliza Mungu aibariki nyumba yao ili imheshimu Kristo. Kila siku waliomba pamoja. Walipopata watoto, watoto nao waliungana na wazazi wao kwa kumwabudu Mungu pamoja kila siku. Jamii yao ya Kikristo ni ushuhuda mkuu kwa ajili ya Mungu.

Hakuna kitu kingine kiwezacho kumsaidia kijana na mkewe ila kuomba pamoja kila siku. Watoto wakizaliwa, ni lazima wakae pamoja na wazazi wao kwa kuabudu. Kwanza mtoto mchanga hataelewa. Lakini mapema mtoto yule atafahamu kwamba huu ni wakati maalumu.

Jamii ikiwa pamoja kwa maombi, Yesu naye atakuwa pamoja nao. (Soma Mathayo 18:20). Ataibariki jamii ile. Kuomba pamoja huwasaidia watu wa jamii kumpenda Yesu zaidi. Pia huisaidia jamii wapendane zaidi. "Jamii iombayo pamoja huishi pamoja."

<u>SEHEMU YA PILI</u>:

Twawezaje kuwa na ibada ya jamii?

Ikiwa bwana yako ni Mkristo, inakulazimu uzungumze naye kuhusu ibada ya jamii. Panga wakati mzuri kwa jamii yako kukutana na kuomba pamoja. Kwa jamii





Tuwafundishe watoto wetu ukweli wa Mungu.

<u>MAOMBI</u>:

Omba ili Mungu atafanya kazi mioyoni mwetu kwa kuondoa woga wote. Dai uwezo wake usimame kwa kumpinga Shetani.

Waombee watu wa Bonde la Mathare walioko Nairobi. Wengi wao hawana chakula wala kazi. Tuiombee Kliniki ya watoto wachanga walio wagonjwa. Mwombee mwuguzi Bi. Nancy Jones pamoja na wale watu wanaomsaidia. Tumwombee mchungaji Patrick Kimani pamoja na shule ya Jumapili. Omba kwamba matoleo ya wanawake Wabatisti wa Kenya yatatumiwa mahali pale kwa kusudi la Mungu.

Mtu huyu alikuja kumwabudu Mungu. Yesu aliwatoa pepo waliokuwa wamempagaa na kumsumbua mtu yule. Watu wengi walisikia habari hizi wakaja kuona wenyewe. Biblia yatwambia kwamba watu wale walimwona yule mtu amevaa nguo na katika akili yake timamu, akiwa ameketi kwenye miguu ya Yesu. (Yapatikana katika Luka 18:26-36.)

Yesu ana uwezo wote, Ana uwezo wa kuwashinda pepo wachafu na pia giza. Paulo alimwandikia Timotheo, akasema, "Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi." (2 Timotheo 1:7.) Tukiogopa uchawi na pepo katika mioyo yetu, uoga huu hautoki kwa Mungu. Watoka kwa Shetani. Yaweza kuwa vigumu kwetu kushinda uoga. Lakini Mungu aweza kuumaliza uoga kutoka mioyoni mwetu. Ni lazima tumwungamie woga huu. Ni Lazima tumwamini ya kwamba anaweza kutuondolea woga huu mbaya.

KIONGOZI:

(Soma Waefeso 6:10-18.) Hivi ni vigumu vya ajabu sana. Tukiwa Wakristo twapigana na Shetani na nguvu za giza. Hatuwezi kupigana na nguvu zetu wenyewe. Twapewa silaha ya Mungu ambayo tutaitumia katika kupigania. Ni lazima tuivae silaha ya Mungu. Kisha tutakuwa na nguvu ya Mungu ndipo tutaweza kuzishinda nguvu za Shetani. Hali tukipigana kila siku na Shetani, huwa twamwomba Mungu. Ni yeye ndiye yule ambaye atashinda vita vyetu na Shetani Mtukuze Mungu! Na tudai ushindi wake.





nyingine, wakati mzuri ni asubuhi. Huabudu pamoja kabla ya baba kwenda kazini na kabla ya watoto kwenda shuleni. Kwa jamii nyingine wakati mzuri ni jioni kabla ya kulala.

Baba Mkristo inambidi aiongoze ibada ya jamii. Ikiwa mumeo si Mkristo, basi itakubidi upange wakati wa kuabudu. Inakubidi uwaongoze watoto wako kuabudu pamoja )awe.

Mkaribishe mumeo. Lakini usijaribu kumlazimisha. Wewe na watoto wako mwaweza kumwombea. Kuabudu kwenu pamoja kwaweza kuwa ushuhuda kwake.

Baada ya kupanga wakati wa kuabudu, usiruhusu jambo lo lote likuzuie usiwe na wakati huu wa kuabudu pamoja na wanao.

SEHEMU YA TATU:

Tufanye nini wakati wa ibada ya jamii? Tutafikiri kuhusu mambo ambayo jamii inahitajika kufanya pamoja.

Kila mara, jamii ilisome Neno la Mungu, ambalo ni Biblia. (Soma 2 Timotheo )̣:15.) Waweza kuvisoma vifungu hivi kutoka kwa kitabu cha shule ya Jumapili au kitabu cha Iwe Nuru. Waweza kusoma kitabu cha Biblia kwa kusoma baadhi ya vifungu kutoka kwa kitabu kile kila siku.

Baba au mama aweza kuisoma Biblia. Watoto wakijifunza kusoma, mmoja wao awe na nafasi ya kusoma siku nyingine.

Mmoja aweza kukisoma kifungu ambacho amejifunza kanisani. Ni jambo zuri kujifunza vifungu kutoka kwa Biblia (Zaburi 119:11.)

Baada ya kuvisoma vifungu hivyo, vieleze vifungu hivyo kwa wale watoto ili waelewe. Wafundishe vile Neno la Mungu lilivyo na maana katika maisha yao ya kila siku.

Watu wa jamii wataomba pamoja. Pengine kila mmoja katika jamii ile ataomba maombi mafupi. Uliza ikiwa kuna mtu kati ya jamii yako ambaye ana jambo maalum linalohitaji maombi. Omba kwa ajili ya mambo haya. Mshukuru Bwana kwa vile wewe na jamii yako mnavyomwelewa.

Wakati mwingine pengine jamii itahitaji kuimba pamoja. Watoto hupenda kuimba. Waweza kuimba baadhi ya nyimbo walizojifunza katika shule ya Jumapili na kanisani. Wakati wa ibada ya jamii unapaswa kuwa wakati wa furaha kwa jamii nzima.

SEHEMU YA NNE:

Kristo ni lazima awe wa kwanza katika maisha yetu. Na tusimulie habari za mwa[illegible]-mke aitwaye Bi. Maposa. Ni Mkristo ambaye mumewe alikuwa hajampokea Kristo.

Bi. Maposa alichukua wakati wa kuwafundisha watoto wake upendo wa Kristo. Alijua ya kwamba mume alihitajika katika ibada ya jamii, lakini mumewe hakuwa Mkristo. Alikuwa na maombi ya jamii na





Alisema kwamba mambo haya yanamchukiza. (Soma Kumbukumbu la Torati 18:10-13 na Kutoka 22:18).

Mfalme Sauli alikuwa mfalme wa watu wa Mungu katika Agano la Kale. Alipochukua cheo cha ufalme, aliwafukuza watu wote waliokuwa wachawi na waaguzi kutoka nchini mwake. Jambo hili lilimfurahisha Mungu.

Baadaye mfalme Sauli alianza kutenda dhambi. Aliacha njia ya Mungu. Mfalme Sauli aliogopa wakati wa kwenda vitani ulipofika. Hakuendelea kuwa na uwezo wa Mungu kwa sababu ya dhambi.

Mfalme Sauli alimwendea mchawi kumwuliza ni jambo gani ambalo litatukia vitani. Mungu alimwaadhibu Sauli kwa dhambi aliyoifanya. Siku ya pili yake vitani, Sauli aliuawa. Watoto wake wote waliuawa vitani siku ile.

Mafundisho ya Mungu ni wazi kwetu. Mungu hataki tuwe na uoga mioyoni mwetu. Hataki tutende dhambi kwa kuwaogopa wachawi na pepo.

SEHEMU YA NNE:

Yesu aliwaponya watu waliokuwa wamepagawa na pepo. Mtu mmoja katika nchi ya Wagerasi aliishi kwenye makaburi. Hakuvaa nguo. Alitumia wakati wake akipaza sauti na kujikwaruza na mawe. Watu walijaribu kumfunga lakini aliikata minyororo aliyofungwa nayo.

lote kuhusu pepo yule. Wakati alipoomba hakujua ya kwamba alitaka pepo yule aondolewe.

Siku ilifika ambapo mwanamke yule alikuwa ni.abatizwe. Kwa ghafula alianza kutetemeka na kupaza sauti. Ilikuwa vigumu kwa waume wawili kuweza kumzuia. Mchungaji alianza kuomba Mungu kumtoa pepo yule. Pepo yule alimtoka naye akaanguka chini na kukaa kwenye ardhi. Mahali Kristo ali poishi, roho za Shetani hazikuweza kuishi. Aliposimama imara kwa Kristo, yule pepo ilimbidi aondoke.

Mchawi mkuu aligeuka na kuwa Mkristo. Alifahamu moyoni mwake kwamba uchawi ni wa Shetani. Hakuendelea kupata mahitaji yake kutokana na fedha alizopata za uchawi. Alifika kanisani hali akiwa amevaa nguo zake za uchawi na vyombo alivyokuwa akitumia kwa kuagua. Alikubali kwamba vyombo vyote vichomwe kwa vile alikuwa ameacha njia zake za dhambi. Alisema kwamba sasa alikuwa na maisha mapya katika Kristo.

Na tuombe kwamba tujue ukweli kuhusu pepo na uchawi. Na tuombe ili Mungu atufanye huru kutokana na dhambi kuu tuliyo nayo katika mioyo yetu.

<u>SEHEMU YA TATU</u>:

Katika Agano la Kale, Mungu aliwapa watu wake amri nyingi. Alisema ya kwamba kusiwe na uchawi au kuamini mizimu au kuwa na watu wake ambao huwaendea pepo.





mafunzo ya Biblia pamoja na watoto wake kila siku. Kwa wakati huu wote aliwafundisha watoto wake upendo wa kanisa. Pia, aliwafundisha kuhusu utoaji wa fungu la kumi kwa kanisa.

Watoto walipoendelea kumpenda Mungu, walitaabishwa na hali ya baba yao. Walimwuliza awe pamoja nao kwa ibada ya jamii. Watoto walianza kumwombea baba yao mmoja mmoja. Walimwuliza baba yao aende pamoja nao kanisani. Kila mara alitoa udhuru tofauti na kukataa kwenda.

Siku moja mchungaji wa kanisa alizungumza na Bw. Maposa. Mchungaji alizungumza kuhusu upendo wa Kristo kwa watu wote. Huu ni upendo mkuu kwa sababu ulimfanya Kristo afe kwa ajili ya wenye dhambi wote. Pale pale yule baba watoto alisema, "Ninaamini, mchungaji. Leo ninajiona waziwazi kwamba ni mtenda dhambi. Najua kwamba Yesu pekee ndiye awezaye kuniokoa. Ninamwamini."

Jumapili iliyofuatia, baba yule alikwenda kanisani pamoja na jamii yake. Alianza kujifunza ili aweze kubatizwa na kuwa mshiriki wa kanisa. Leo kuna furaha kuu katika nyumba ya mtu huyu.

<u>KIONGOZI</u>:

Ni muhimu kuwa na wakati maalumu wa ibada ya jamii nyumbani. Jambo hili litawasaidia watoto wenu wakue kama Wakristo. Jambo hili litaiimarisha nyumba zenu. Ikiwa huna ibada ya jamii, fikiria kuhusu

mambo haya. Omba ukimwuliza Mungu akusaidie uwe na ibada ya jamii.

MAOMBI:

Omba ili Mungu atusaidie tuwe na ibada ya jamii katika nyumba zetu.

Waombee Wanawake Wabatisti wa Kenya watakapokutana katika Juma la kwanza la mwezi wa Februari. Omba kwamba Roho Mtakatifu wa Mungu atamwongoza mwenye kiti, yaani Bi. Elizabeth Muriu, pamoja na wale viongozi wengine. Omba kwamba wanawake watahuishwa katika mambo ya kiroho.





Mwalimu wao aliwauliza ikiwa walimwamini Mungu, Mungu pekee wa kweli. Wanafunzi hawa walijibu ya kwamba wanaamini. Aliwauliza wafunge macho. Aliwauliza wote wale ambao hawawaogopi wachawi wanyoshe mikono yao. Katika darasa zima la sita, watatu kati ya wanafunzi wote ndio walionyosha mikono yao.

Kwa nini wanafunzi wa Kikristo bado anawaogopa wachawi? (Waruhusu wanawake wajadiliane kuhusu swali hili.)

Ni ukweli gani ambao uko katika uchawi? Biblia yatufundisha kwamba ni kazi ya "Mwili" au Shetani. Watu wanaoufanya uchawi hawana nafasi katika ufalme wa Mungu. (Soma Wagalatia 5:19-21).

Twajua kwamba tukiwa Wakristo ni lazima tupigane na Shetani katika nguvu ya Roho Mtakatifu. Yesu amemshinda Shetani. Yesu atafanya kazi katika maisha yetu ili tumshinde. Tukiwa waoga, twaweza kumwungamia Yesu dhambi yetu hii ya uoga. Twaweza kumwuliza atuondolee. Twaweza kudai uwezo wake ili tumshinde Shetani maishani mwetu.

SEHEMU YA PILI:

Ni jambo gani ambalo hutukia kwa mtu ambaye hupagawa na Shetani na kisha kumpokea Kristo? Ni jambo gani hutukia kwa mchawi ampokeaye Kristo? Mwanamke mmoja aliyekuwa na pepo mwenye nguvu alithibitisha wa dhambi. Alimwamini Yesu kama Mwokozi. Alimwuliza mchungaji amwombee ili Mungu amwondolee mambo yote. Hakujua lo

## SHIDA ZA NYUMBANI: WOGA

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:
Siku ya hofu yangu nitakutumaini wewe. Zaburi 56:3

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Leo twaanza somo kuhusu uoga na dini ambako huleta shida nyingi nyumbani mwetu. Baadhi ya shida hizo ni kuogopa pepo, uchawi na ramli na kadhalika.

Hali tunajifunza, na tuombe ili Mungu asimulie ukweli katika mioyo yetu. Yesu alisema, "Tena mtafahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru" (Yohana 8:32).

Kifungu chetu cha kukumbuka cha leo kinatwambia kwamba hali tunamsikiliza Mungu atatupa uhuru kutokana na uoga wa uovu. Tunamwuliza Bwana atufundishe ukweli. Tunamwuliza atuweke huru kutokana na ile aina mbaya ya uoga.

SEHEMU YA KWANZA:

Wanafunzi katika shule ya Kibatisti walikuwa wanajifunza kuhusu Mungu na uwezo wake mkuu. Walianza kuzungumza kuhusu vile watu wawaogopavyo wachawi.





## KUWATUNZA WATOTO

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:
Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyosha mapito yako.
Mithali 3:5, 6

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

Maelezo Kwa Kiongozi:

Waweza kumwalika mwuguzi au daktari au mwalimu kutembelea mkutano wenu wa wanawake na kuufundisha mpango wa leo. Waweza kuipata orodha ya vyakula kwa watoto kula. Wakati mwingine shule au kiliniki huwa na orodha hizi.

UTANGULIZI:

Wakina mama wana kazi nyingi za kufanya nyumbani. Ni kazi yetu kuwatunza watoto wetu. Ni kazi yetu kuwaweka safi na nadhifu. Ni kazi yetu kuwafundisha jinsi ya kuitunza miili yao. Ni kazi yetu kuwafundisha umuhimu wa kuwa safi.

Sisi pia huwafundisha watoto wetu kufanya kazi na kuifanya kazi hiyo vizuri. Wakiwa shuleni, sisi huwabidisha wajifunze kwa bidii na kufanya vizuri masomoni.

Huwafundisha adabu njema.

Wakina mama wana kazi muhimu ya kuwapa watoto wao chakula bora. Inatubidi tuhakikishe ya kwamba wanakula vyakula vinavyohitajika kwa kuifanya miili ikue ikiwa yenye nguvu. Haya ni baadhi ya mambo ambayo tutajifunza leo.

SEHEMU YA KWANZA:

Mama mmoja alimleta hospitalini mtoto wake aliye na umri wa miaka mitatu. Nyanya ya mtoto yule alikuwa ameulizwa apewe mtoto yule wakati alipokuwa na umri wa miaka miwili. Kwa mwaka mmoja, mtoto yule alikuwa ameishi na nyanya yake.

Nyanya yule hakujua jinsi ya kumlisha yule mtoto. Alimlisha mjukuu wake ugali na uji. Wakati mwingine alikuwa na mboga. Hakumlisha mayai au maziwa. Alimlisha kiasi kidogo tu cha nyama.

Baada ya miezi michache, yule mtoto alipatwa na ugonjwa wa kuhara. Nyanya yake alimtengenezea dawa, lakini ugonjwa huo haukutibika. Baadaye alimpeleka mjukuu wake katika kiliniki. Bado kidogo mtoto yule alianza kupona. Lakini yule nyanya ya mtoto hakumpeleka tena kufanyiwa uchunguzi zaidi na daktari.

Nywele za mtoto yule zilibadilika na kuwa nyekundu na pia nyembamba. Nywele zenyewe zilinyoka. Ngozi yake ilikuwa nyeupe. Kisha mikono yake na miguu ilianza kufura. Alikuwa na tumbo iliyofura.





mnamo mwezi wa Machi. Tumwombe Mungu ili awaongoze kutoa kwa ukarimu kwa ajili ya kazi yake.

TANGAZO!

Hakuna mpango wa kwanza katika juma la kwanza la mwezi wa Machi kwa sababu ni Juma la Maombi, yaani tarehe 3-9. Wiki ıii someni Masomo ya Juma la Maombi.

Na tumwulize Mungu atupe ndimi za ufadhili na upendo.

KIONGOZI:

Mungu ataka kumwonyesha kila mtu upendo wake. Katika I Wakorintho 13:4-8, twaona tabia ya aina hii ya upendo:

"Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na ukweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma, yakiwapo maarifa, yatabatilika."

Natumwulize Mungu atupe aina hiyo ya upendo nyumbani mwa kila mmoja!

MAOMBI:

Na tuombe ya kwamba tuwe na upendo wa Mungu mioyoni mwetu na nyumbani.

Na tuombe ili tutakuwa na mawazo mazuri kuhusu fedha.

Na tuombe ili tuweze kutoa fungu la kumi kwa Mungu ambalo ni mali ya Mungu na kanisa Lake.

Tuombe kwamba Wanawake Wabatisti wa Kenya na Tanzania wayatoe matoleo yao kwa njia ya ukarimu katika Juma La Maombi,





Alikuwa mwenye chuki na mchovu na mnyonge sana wa kukimbia na kucheza. Tumbo ya kuhara damu ilimshika tena.

Kisha yule nyanya ya mtoto alimpeleka kwa mama yake. Mama wa mtoto yule alimpeleka kwa haraka hadi hospitalini. Ilikuwa vigumu kumponya mtoto yule tena.

Ugonjwa wa mtoto yule ulistawi kwa sababu hakupewa chakula kizuri. Ilikuwa vibaya zaidi kwa sababu alikuwa na minyoo pia.

Siku hizi, kuna watoto ambao wana hali kama ya mtoto huyu. Hawali vyakula bora. Wakati anapokuwa na nywele nyembamba, zilinyoka, nyekundu, halishwi vyakula vilivyo bora. Kisha ngozi yake huwa nyeupe. Baadaye mwili huvimba isipokuwa awe ametibiwa.

SEHEMU YA PILI:

Twataka watoto wetu wawe na miili yenye afya nzuri. Kuwalisha watoto wetu vizuri ni sehemu muhimu ya kazi yetu.

Kukua vizuri, watoto wanapaswa kuwa na vyakula mbalimbali. Ni lazima wawe na vyakula kama samaki, nyama, mayai, n.k. Ugali na uji wa mahindi si chakula kizuri kwa watoto wadogo. Tutajifunza kuhusu chakula katika sehemu ya nne.

Ni muhimu kuviweka vyakula na vyombo katika hali ya usafi. Inabidi viwekwe mbali na mainzi. Mainzi hubeba magonjwa

ambayo huwafanya watoto wetu kuwa wagonjwa sana. Vyombo vya chakula vinapaswa kuoshwa na maji ya moto. Kisha kifunikwe yasije mainzi yakatua juu yake. Inatubidi tuwafundishe watoto wetu waioshe mikono yao vizuri kabla ya kula.

SEHEMU YA TATU:

Ni muhimu kuwapeleka watoto wetu katika kiliniki za watoto au kiliniki nyingine. Inatubidi tuwapeleke watoto kwenye kiliniki wakiwa na umri wa mwezi mmoja. Uliza katika kiliniki kuhusu sindano ya kuwazuia watoto wachanga na wakubwa kutoshikwa na magonjwa mabaya. Sindano hizi kuanza kupigwa watoto wakiwa na umri wa mwezi mmoja hadi mitatu, na ni lazima mtoto apigwe sindano nyingi. Sindano zote ni lazima apigwe mtoto wako. Ikiwa una watoto ambao hawakupigwa sindano hizi, wapeleke kwenye kiliniki kwa sindano hizi.

Sindano hizi hukinga magonjwa kama vile surua, ndui, kupooza, kifaduro, pepo punda, ugonjwa wa koo ndani wa kuambukiza na kifua kikuu. Katika kiliniki zungumza na wauguzi wa kike au daktari. Uliza kuhusu njia bora za kuwalisha na kuwatunza watoto wako au mtoto wako mchanga. Watakuwa tayari kukusaidia.

Pia ni muhimu kuwapeleka watoto wachanga na wakubwa katika kiliniki au hospitali wakati wakiwa wagonjwa. Wakati mwingine wakina baba hulazimika kufanya kazi mbali na nyumbani. Kabla ya kuondoka,





ya Mungu katika kukutana na shida.

"Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa. Ila na aombe kwa imani...." (Yakobo 1:5,6). Hii ni ahadi moja ya Mungu. Tukimwuliza, atatupa busara ambayo itatujulisha la kufanya wakati wa shida.

Mke wa Kikristo amwombe Bwana kwa nguvu. Ni lazima amwombee mumewe ili naye awe Mkristo. Ni lazima amwombe Mungu nguvu na busara. Ni lazima amwulize Mungu amsaidie ili aishi maisha yaliyo sawa na awe mwema na mwenye kupenda. Ni lazima amwombe Mungu amsaidie katika kumshuhudia mumewe.

SEHEMU YA NNE:

Bila shaka, kuna mambo mengine ambayo yaweza kuleta shida nyumbani. Jambo kubwa zaidi ni ulimi mwovu. Ulimi mwovu waweza kuleta chuki nyingi.

Tukizungumza na hasira au kugombana, twaweza kuwaudhi bwana zetu. Ulimi wa ugomvi waweza kuleta chuki. (Soma Mithali 21:9). Amani nyumbani yaweza kumalizwa na ugomvi.

Dhambi nyingine ni ile ya kueneza uvumi. (Soma Mithali 17:9.) Mara nyingi inaonekana kwamba wanawake wengi hujaribiwa watende dhambi katika njia hii.

Njia ya Mungu ni kwa Mkristo na mkewe kupanga pamoja. Mume ndiye kichwa cha Nyumba, na mke inambidi ampende na kumheshimu mkewe. Inambidi asiwe mchoyo wa fedha. Twaona ya kwamba tatizo la fedha laweza kuwa baya sana kwa nyumba.

SEHEMU YA TATU:

Bw. na Bi. Fodie walikuwa si Wakristo. Bw. Fodie alikuwa na hamu kuu ya utajiri. Mwezi mmoja baada ya kupata mshahara wake, alikwenda kucheza karata. Upesi, aliona ya kwamba fedha zote alizokuwa nazo zimemalizika kwa sababu ya mchezo wa karata. Aliogopa kurudi nyumbani. Akajificha msituni. Mwishowe aliazimia kurudi nyumbani. Alipofika yeye na mkewe walipigana.

Bi. Fodie alitatizika sana. Watoto hawakuwa na chakula. Aliazimia kutafuta kazi ili apate fedha za kununulia chakula. Alipopewa fedha, alizificha. Kulikuwa na shida nyingi katika nyumba hii.

Baadaye, Bi. Fodie aliazimia kumwacha mumewe. Hili ni jambo baya ambalo huleta shida kwa watoto.

Wafikiri jibu la shida za nyumba hii ni nini? (Waulize wanawake wajadiliane shida hii.)

Twajua kwamba Mungu aweza kuwa nguvu yetu kuu katika wakati wetu wa shida. "Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utaonekana tele wakati wa mateso." (Zaburi 46:1). Mkristo aweza kudai nguvu





inambidi mke amwulize mumewe ruhusa ili awapeleke watoto kwa daktari wakiwa wagonjwa. Watoto wengi wadogo hufariki kwa sababu mama yao huwa mwoga kuwapeleka watoto kwenye kiliniki wakati baba yao akiwa mbali na nyumbani.

SEHEMU YA NNE:

Tutajifunza kuhusu baadhi ya vyakula kwa watoto wachanga na wakubwa. Bila shaka, katika mpango mmoja hatuwezi kujifunza kila kitu kuhusu jinsi ya kuwalisha watoto wetu. Ikiwa una maswali mengine zungumza na mmoja wa watu walioko kwenye kiliniki na mwulize akupatie msaada.

1. Maziwa. Maziwa ni chakula muhimu kwa watoto wachanga na wakubwa. Mama inambidi amnyonyeshe mtoto wake mchanga kwa muda mrefu iwezekanavyo. Ikiwa huwezi kumnyonyesha, basi mtoto ni lazima apewe maziwa ya ng'ombe. Maziwa mabichi ni lazima yachemshwe katika chombo safi kwa muda wa dakika ishirini. Kisha maziwa hayo yamiminiwe katika chupa ambazo zimeoshwa na maji ambayo yamechemshwa. Watoto wakubwa wanaweza kunywa kwa kutumia vikombe safi.

Ikiwa huwezi kumkamisha ng'ombe au mbuzi, basi itakubidi ununue maziwa. Maziwa ya unga ni mazuri na ya bei rahisi kuliko maziwa mabichi. Hakikisha ya kwamba unafuata njia za kuyachanganya. Hakikisha ya kwamba maji yamechemshwa kisha kuyaacha yapoe kabla ya kuyachanganya na maziwa ya unga. Watoto wa umri wo wote

waweza kunywa maziwa ya aina hii.

Watoto wachanga kidogo na wakubwa wanahitaji wakia 32 za maziwa kila siku. Kiasi cha maziwa haya ni chupa nne tele, au vikombe vinne.

2. Mayai. Mtoto aweza kuanza kula sehemu ya manjano ya yai akiwa ana umri wa miezi mitano. Itenge sehemu ya manjano kutoka kwa lile yai lililochemshwa. Liponde ponde kwa kutumia uma. Uchanganye unga wa yai hilo na uji pamoja na maziwa. Mtoto aweza kula sehemu ya manjano ya yai kila siku. Mtoto ambaye ana umri upatao miezi tisa aweza kula sehemu nyeupe ya yai na pia ile ya manjano. Aweza kula yai zima kila siku.

3. Nyama. Nyama kwa watoto ni lazima zipikwe vizuri na kukatwa vipande vidogo-vidogo mpaka iwe laini. Mtoto wa miezi mitano aweza kulishwa nyama laini zilizo-pikwa. Afikapo umri wa miezi tisa hadi mwaka mmoja, inambidi ale nyama nzuri zilizopikwa. Ingekuwa vizuri zaidi kama mtoto angekula nyama kila siku, lakini asikose kula nyama mara tatu kila wiki. Kuku, sungura, nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na samaki, zote ni nyama nzuri kwa watoto.

SEHEMU YA TANO:

Katika sehemu hii twaendelea kujifunza kuhusu vyakula kwa watoto.





mshahara ule.

Kwanza Bw. Dube huchukua sehemu ya kumi kutokana na mshahara wake. Huchukua sehemu ya Kumi yaani Sh. 42/- na kupeleka kanisani. Sehemu ndogo ya Sh. 42/- hizi hupewa watoto ili wakatoe sadaka kanisani. Sadaka nyingine itatolewa na Bw. na Bi. Dube kanisani. Lakini fungu lote la kumi litatolewa kanisani mwezi ule.

Kisha Bw. na Bi. Dube huzungumza kuhusu jinsi ya kuzitumia fedha zilizobaki. Watalipia kodi ya nyumba na matumizi mengine. Watatumia kiasi cho chote ambacho kitahitajika kwa chakula. Watakubaliana ikiwa watatumia kiasi fulani kwa kununua nguo na vyombo vingine. Wao ni waangalifu katika kuzitunza fedha zao.

Nyumba hii ina amani na mapatano kati ya wazazi.

SEHEMU YA PILI:

Bw. na Bi. Phiri wote husema ni Wakristo. Lakini amani na furaha inakosekana nyumbani kwao. Bi. Phiri hufanya kazi kila mwezi. Husema ya kwamba fedha za shahara wake ni zake pekee. Hutaka kuzitumia binafsi.

Hakuna **hata** mmoja kati ya Bw. au Bi. Phiri ambaye hufikiria kuhusu fungu la kumi. Kila mmoja anashughuli nyingi akifikiria mambo mazuri ambayo anataka kujinunulia. Ndani ya mioyo yao wanafahamu ya kuwa wanamwibia Mungu. Lakini hawatamsikiliza Mungu! Wanazipenda fedha sana.

## MATATIZO AMBAYO HULETA HUZUNI NYUMBANI

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:

> Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha.
> 1 Timotheo 6:10

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Kuna matatizo mengi majumbani siku hizi. Tutajifunza baadhi ya matatizo hayo.

(Soma I Timotheo 6:7-10).

Matatizo kuhusu fedha yaweza kusababisha shida nyingi nyumbani. Watu wengine wanapenda fedha zaidi kuliko wanavyopenda kuifurahisha jamii yao. Pia, watu wengine hupenda fedha sana kuliko Mungu. Kupenda fedha zaidi husababisha mtu kuwa mchoyo na mwenye moyo mgumu. Hii si njia ya Mungu. Huleta chuki nyingi. Vifungu vya maandiko tunavyovisoma vinatuambia kwamba fedha husababisha "Kujichoma moyo kwa maumivu mengi," (Kifungu cha 10.)

SEHEMU YA KWANZA:

Bw. na Bi. Dube ni mtu na mkewe na ni Wakristo wawili wenye furaha. Bw. Dube ni mwalimu. Kila mwezi hupokea Sh. 420/-. Bw. Dube akiuleta nyumbani mshahara wake, yeye na mkewe huzungumza pamoja juu ya





4. Uji. Uji wa ngano waweza kulishwa watoto wachanga wakati wakiwa na umri wa miezi miwili hadi mitatu. Anza kumlisha kiasi kidogo kikichanganywa na maziwa. Mpe mtoto kiasi zaidi wakati akiendelea kujifunza kuula uji huo. Uji uliotengenezwa kutokana na unga wa mahindi zi chakula kizuri kwa watoto wachanga.

5. Mboga. Hizi ni nzuri kwa watoto na inawapasa wazile kila siku. Maharagwe na mbaazi ni chakula kizuri kinachoijenga miili ya watoto.

6. Matunda. Watoto walio na umri wa miezi kama miwili waweza kupewa maji ya machungwa. Ndizi mbivu zilizopondwa-pondwa ni nzuri kwa watoto walio na umri wa miezi mitano hadi sita. Watoto wakikua na kuwa wakubwa kidogo inawabidi wawe na aina nyingine ya matunda.

7. Siagi ya Njugu. Hiki ni chakula kizuri kwa watoto wakubwa. Watoto wadogo hawastahili kupewa njugu. Hizi zaweza kuingia katika bomba la kuvutia pumzi na kuingia kwenye mapafu. Hii ni hatari sana.

KIONGOZI:

Bila shaka, bado hatujaweza kujifunza vizuri mambo haya yote. Ikiwa una maswali yo yote hakikisha ya kwamba unawauliza watu walioko kwenye kiliniki wakati unapompeleka mtoto wako kwa matibabu. Tukiwa wakina mama Wakristo, twataka kuwasaidia watoto wetu katika kila njia.

MAOMBI:

Mshukuru Mungu kwa watoto ambao anawapatia katika nyumba zenu. Mwombeni ili awapatie nguvu yake hali mkiwa mnawatunza watoto hao. Omba ili wakue na kumtukuza Kristo na maisha yao.

Tuiombee Bible School (Shule ya Biblia) iliyoko katika Mbale, Uganda, pamoja na kumwombea mwalimu wake, Bw. Washington Masete. Waombee Wachungaji wa Kibatisti katika Uganda ili waweze kuendelea katika kuihubiri Injili. Tuwaombee Wamisheni wanne wa Kibatisti walioko Jinja na Moroto.





John na Kathy Dillman, wanaojaribu kuanzisha mpango wa kuwashuhudia Wamasai.

uwezo wake ili uwe huru kutokana na wivu. Mwulize akupe upendo wake kwa watu wote katika nyumba yako.

Ikiwa wewe ni mke mmoja tu nyumbani, usimshawishi mumeo aoe mke mwingine. Wake wengine hufanya hivi. Hutaka kuwa mahakimu wa mke wa pili. Usimkubalie mumeo aoe mke wa pili. Uwe mwaminifu kwake. Jaribu kumfurahisha maisha yake. Omba ili Mungu akusaidie katika nyumba yako.

KIONGOZI:

Na tufikirie tena kifungu cha kukumbuka, 1 Wakorintho 10:13. Twaweza kujaribiwa tufanye uasherati. Lakini twaweza kudai ahadi ya Mungu kutukomboa. Mwanamke mmoja alitoa ushuhuda wake katika mkutano wa jumuiya. Alisema kwamba kabla ya kuwa Mkristo mwili wake ulikuwa na tamaa ya uasherati. Aliendelea kumtegemea Mungu kumtoa kutokana na tamaa ile mbaya ya uasherati. Uwezo wa Mungu watosha! Twaweza kuudai. Wakati wo wote tunapojaribiwa na Shetani, twadai ushindi kutoka kwa Kristo.

MAOMBI:

Ombeni pamoja kwamba Mungu azibariki nyumba zetu. Ombeni ili tuwe na uwezo Wake ambao utatufanya tuyashinde majaribu ya kila aina.

Tuyaombee makabila ambayo hayajamwamini Yesu kwa wingi. Tuombe njia ipatikane ya kuwashuhudia. Tuwaombee wamisheni,





## KUWASAIDIA WATOTO WETU WAJITAYARISHE KWA UTU UZIMA

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:
Mkinipenda, mtazishika amri zangu.
Yohana 14:15

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Leo tutajifunza zaidi kuhusu wajibu wetu kama wazazi wa Kikristo. Tumeshasema ya kwamba Mungu hutupa watoto. Tuko nao kwa muda wa miaka michache. Kwa muda huu mfupi ni lazima tuwatayarishe watoto hao kwa utu uzima. Twawataka wapate furaha katika maisha yao.

Paulo alimwandikia Tito kwamba wanawake wazee ni lazima wawafundishe wanawake vijana (Tito 2:3,4). Kuna mambo mengi ambayo twaweza kuwafundisha watoto wetu.

SEHEMU YA KWANZA:

Mtoto wa Kikristo alikuwa amemwacha Bwana Mungu. Alifikiri ya kwamba mambo ya ulimwengu yangemletea furaha. Aliona ya kwamba uvutaji, unywaji hakukumletea furaha. Aliona ya kwamba alikuwa ameiacha furaha ya kweli alipomwacha Bwana Yesu.

Mtoto huyu alitubu hali machozi yakimtoka. Alisema, "Njia ya Kristo ndiyo njia ya pekee ya furaha. Kila mara inatubidi tufundishe ya kwamba sheria ya Mungu huleta furaha ya Mungu maishani." Aliirudia tena njia ya Bwana.

Tuzo zuri zaidi ambalo twaweza kuwapa watoto wetu ni kuwafundisha habari za Yesu. Inatubidi tuanze kuwafundisha wakati wakiwa wadogo sana. Inatubidi tuendelee kuwafundisha kila siku wakiwa nyumbani.

Inatupasa kuwasaidia watoto wetu wajue kwamba Mungu atawaongoza. Inatupasa tuwafundishe kuomba wakati wakiwa na majaribu. (Soma 1 Wakorintho 10:13). Inatupasa tuwafundishe jinsi ya kumwuliza Mungu mambo ambayo wanastahili kuyafanya na maisha yao. Inatupasa tuwafundishe jinsi ya kuomba kuhusu uamuzi wo wote watakao kuufanya. Tukiomba pamoja nao, wao hujifunza. Wakitusikia tukiomba kwa uongozi, wao hujifunza.

SEHEMU YA PILI:

Marafiki wa watoto wako ambao wanao ni wa maana sana. Hakikisha ya kwamba unawajua marafiki wao. Wasaidie watoto wako wajue jinsi ya kuchagua marafiki wazuri.

Hakikisha ya kwamba unafahamu watoto wako walipo. Usiwaruhusu wazunguke ovyo mjini au mwituni wakati usipojua waliko. Uwasisitize wawe wasikizi, hata





Twajua ya kwamba Pepo hawezi kusababisha vifo. Walakini, watu wanaoamini pepo huzungumza mengi. Huleta huzuni nyingi kwa wengine. Hakutakuwa na amani kwa mke wa kwanza katika kijiji kile.

SEHEMU YA NNE:

Kuoa zaidi ya mke mmoja pia huwaletea watoto shida. Mara nyingi baba atawaelimisha watoto wa mke wa kwanza peke yao. Watoto wa mke wa kwanza waweza kupewa chakula kizuri na nguo. Watoto wa mke wa kwanza hurithi mali ya baba yao.

Mambo haya yote huleta wivu kati ya watoto. Watoto waweza kuchukiana. Watoto wa mke wa pili waweza kukubaliana kuwapiga watoto wa mke wa kwanza. Wanaweza kukosa mahitaji yao mengi kwa sababu hakuna fedha za kutosha.

Kuoa zaidi ya mke mmoja huvunja ndoa safi iliyopangwa na Mungu. (Soma Mathayo 19:5,6). Kuoa zaidi ya mke mmoja siyo njia ya furaha na amani kwa nyumba.

SEHEMU YA TANO:

Ni jambo gani ambalo mwanamke aliyeolewa na mume aliye na zaidi ya mke mmoja aweza kufanya?

Katika Waefeso 4:32 twafundishwa kuwa wafadhili sisi kwa sisi. Katika Warumi 12:18 twajifunza tuishi kwa amani na watu wote. Mwulize Mungu akupe nguvu yake ili uwe mfadhili. Mwulize akupe

Mpango wa Mungu kwa jamii huleta furaha. Na tuwafundishe watoto wetu mpango wa Mungu.

SEHEMU YA TATU:

Kuoa zaidi ya mke mmoja si mpango wa Mungu kwa ndoa. Hakuna "mwili mmoja." Kuna watu watatu, mapenzi mara tatu, roho tatu, nyumba tatu. Kuoa wake zaidi ya mmoja huleta shida na chuki, kama tulivyoona katika hadithi ya Yakobo.

Kuoa zaidi ya mke mmoja kwaweza kuharibu uhusiano ulioko kati yao. Kila mke hujaribu njia zo zote za kumfanya mumewe ampende. Wengine hutumia dawa za mapenzi. Wake wengine hutumia uchawi. Wengine waweza kumtilia sumu mke mwingine ili afe. Dawa nyingine za mapenzi zaweza kumfanya mume awe mtu bubu na kumfanya asifikirie jambo lo lote. Kuna mashaka mengi nchini ambayo huletwa na dhambi hii ya kuoa zaidi ya mke mmoja. Kuna chuki nyingi kwa kuoa wanawake iletwayo na dhambi hii.

Msichana aliyeolewa alifariki alipozaa mtoto. Watu walieneza habari ya kwamba yule mke wa kwanza ndiye aliyesababisha kifo kile. Yule mke wa kwanza alipata shida nyingi kwa sababu ya habari hii. Mwaka uliofuata mke huyo wa kwanza alimzaa mtoto aliyekuwa amefariki tayari. Watu walisema kwamba roho ya yule mke aliyekuwa amekufa ndiyo iliyesabisha jambo lile.





kwa wakubwa zao wa nyumbani.

Usiwaruhusu watoto wako kukaa bure bila kazi. Ikiwa hawana kazi, wape kazi ya nyumbani. Wahimize wajifunze wakiwa nyumbani. Hakikisha ya kwamba wanaenda pamoja nawe katika shule ya Jumapili na kanisani.

Lisaidie kanisa lako kupanga mambo ambayo watoto wadogo watafanya. Ongea na mchungaji na mashemasi juu ya jambo hili. Panga mikutano ya vijana. Wapangie kuwa na michezo ya Kikristo. Maisha ya Kikristo ni maisha ya furaha. Saidia kulifanya jambo hili liwe la kweli kwa vijana.

SEHEMU YA TATU:

Vijana hukutana na majaribu mengi. Ni lazima tuwafundishe njia za Kikristo. Ni lazima tuwafundishe sheria za Mungu. Ni lazima tuwafundishe kumpenda Yesu kwanza na kuheshimu sheria zake. (Soma kifungu cha kukumbuka cha leo.) Watoto wawezaje kuwa wenye nguvu? Twawezaje kuwasaidia wajue mambo yaliyo ya haki?

Siku zote waambie watoto ukweli. Wakiuliza kuhusu watoto wachanga, waeleze vile Mungu alivyompangia mwanamke kuwa mama. Mungu aliifanya miili yetu katika njia ya ajabu. Wasichana hukua ili wawe wakina mama. Wavulana hukua ili wawe wakina baba. Ni mpango wa Mungu kwamba wakati wanapokua na kuoa wale wanaowapenda, watawapata watoto na kuwa na nyumba yao. Ni mafundisho ya Mungu kwamba bwana na

mwanamke wasilale pamoja isipokuwa wame-oana.

Mabadiliko yatukiayo katika miili ya wavulana na wasichana ni yenye uwezo sana. Mabadiliko haya yanaweza kumfanya mtu aangukie dhambini. Ni sawa kwa wavulana na wasichana kupendeleana. Lakini ni lazima tuwafundishe watoto wetu wailinde miili yao ili iwe safi kwa uangalifu sana. Msichana ni lazima afundishwe kukataa kwa nguvu wakati mvulana anapotaka kuugusa mwili wake. Ni lazima afundishwe kwamba njia ya furaha katika maisha yake ya kuolewa ni kujiweka safi kwa ajili ya bwana yake.

Wasichana ni lazima wasifanye mambo ambayo watawavuta wavulana kutenda dhambi na miili yao. Wasichana ni lazima wavae kwa uangalifu. Mavazi mafupi yanayokaba mwili na yale ambayo yaonyesha matiti huwavutia wavulana. Wavulana na wasichana ambao hukumbatiana na kupeana busu kila mara hujaribiwa kutenda dhambi.

Tukiwa wazazi wa Kikristo ni lazima tuwafundishe watoto wetu mambo haya yote. Ni lazima tuanze kuwafundisha wakati wakiwa bado wadogo.

SEHEMU YA NNE:

Ni lazima tuwafundishe watoto wetu kwamba dhambi itaadhibiwa (Hesabu 32:23). Twaweza kuwafikiria wasichana ambao maisha yao yameharibika kwa sababu ya dhambi ya usherati.





SEHEMU YA PILI:

Mkristo mmoja alikuwa na mke aliyekuwa ni tasa. Aliwataka watoto wake wenyewe. Alitaka kuoa mke wa pili. Alisema, "Watu wa Agano la Kale walikuwa na wake zaidi ya mmoja."

Walakini, waliendelea kujifunza Neno la Mungu. Aliona kwamba kuwa na zaidi ya mke mmoja haukuwa mpango mzuri wa Mungu. Mwanamume aliingia katika njia ya dhambi wakati alipojizoeza kuwa na zaidi ya mke mmoja. Dhambi hii kila mara ilileta chuki nyumbani.

Tutaona hadithi moja kati ya zile jamii za Agano la Kale. Mtu mmoja aliitwa Yakobo. Aliwaoa dada wawili, Lea na Raheli. Lea alimwonea Raheli wivu kwa sababu Yakobo alimpenda Raheli zaidi kuliko Lea. Raheli alimwonea Lea wivu kwa sababu Lea alikuwa na watoto wengi. Wakati wote mlikuwa na chuki katika nyumba ile.

Mwishowe Raheli alipata mtoto wa kiume, Yusufu. Sasa Yakobo alimpenda Yusufu kuliko wale watoto wake wengine. Watoto wake wengine walimwonea Yusufu wivu. Walimchukua Yusufu na kumwuza kama mtumwa. Yakobo alikuwa na majonzi sana moyoni mwake kwa sababu wanawe wengine walimwambia kwamba Yusufu alikuwa amefariki. Dhambi ilileta huzuni nyingi na chuki. Yakobo alikuwa hana furaha. Wake zake hawakuwa na furaha. Watoto wake hawakuwa na furaha pia.

ni dhambi mbili kuu kabisa ambazo huleta shida nyingi nyumbani.

SEHEMU YA KWANZA:

(Soma 1 Wakorintho 6:15-20).
Uasherati huharibu mwili. Ni dhambi ya mwili. Mwili wa Mkristo ni hekalu la Roho wa Mungu. Inamlazimu mtu auweke safi kutokana na dahmbi ya aina yo yote. Wanawake, mwili wenu si mali yenu binafsi! Yesu Kristo amekununua kwa ajili yake na damu yake. Na uwezo wake, jiweke safi!

Uasherati huleta shida nyumbani. Kutakuwa na ugomvi mwingi hata kupigana. Furaha ya nyumbani huharibika. Talaka na kifo cha nyumba ile chaweza kutukia.

Mwanamke Mkristo, ni lazima awe mke wa haki kwa mumewe. Mwanamke Mkristo humtaka mumewe awe mwenye furaha. Hataki mumewe awe na hamu ya kulala na mke mwingine.

Si vizuri kwa mume na mke kutengwa kwa muda mrefu. Jambo hili huwafanya waingilie uasherati. Twawajua waume wengi wanaofanya kazi katika miji mikuu na wake zao wanaishi mijini na wengine wanaishi huko kwao vijijini. Jambo hili ni makosa sana. Ikiwezekana, mke na mume inawabidi waishi pamoja. Watoto pia wanawahitaji wazazi wote wawili.





Msichana mmoja alitiwa mimba na mvulana aliyeahidi kumwoa. Walakini, hakutimiza ahadi yake. Jambo alilotaka ni ule mwili wa msichana. Kisha alimwacha. Aliulizwa kwa nini alimkubalia mvulana yule. Alisema, "Aliniambia ya kwamba ikiwa kwa kweli ninampenda, ningejitoa kwake."

Alikuwa ni msichana wa Kikristo. Alijua kwamba ni lazima amweke Yesu kwanza maishani mwake. Yesu alisema, "Ukiwa wanipenda, utayaweka maagizo yangu. "Msichana yule alitenda dhambi. Aliadhibiwa. Maisha yalikuwa magumu kwake. Hakupata furaha katika dhambi yake. Alipata majonzi.

Wafundishe watoto wako kwamba njia ya maisha ya furaha ni kumcha Mungu.

SEHEMU YA TANO:

Wakati watoto wetu wakiwa tayari kwa ndoa, inatubidi tuwasaidie. Twafahamu wakati mwingi ambapo mvulana alikuwa ameanza kulipa mahari. Kisha wale wazazi wa msichana wakaendelea kuongeza kiasi cha fedha za mahari. Jambo hili lilimfanya yule mvulana asiweze kulipa. Alichoka kungojea muda mrefu ndipo apewe yule msichana. Walianza kulala pamoja, kisha wazazi wa mvulana waligharimiwa uharibifu. Wazazi walifanya makosa katika kukifanya kiasi cha mahari kiwe kikubwa zaidi hata kuwafanya wapenzi wawili wangojee kwa muda mrefu kabla ya ndoa kufanywa.

Tukiwa Wakristo, na tujaribu kufikiria jambo zuri kwa watoto wetu. Natuja-

ribu kuwasaidia na si tu kuziongeza pesa zetu wakati wa ndoa. Natuwasaidie watoto wetu wawe na ndoa za Kikristo.

KIONGOZI:

Ni lazima tuombe sana ili Mungu atusaidie sisi wakina mama tuweze kuwafundisha watoto wetu njia yake. Na tuwe na wakati wa maombi sasa, tukimwuliza Mungu atupatie uongozi wake katika nyumba zetu.

Maombi:

Waombee waandishi wa vitabu vya Kikristo, hasa wale wanaotunga Masomo, Iwe Nuru, Ujumbe na vitabu vingine. Omba kwamba wataweza kuandika kwa njia ambayo itawasaidia wasomaji kufahamu zaidi juu ya Ukristo. Waombee watenda kazi wa Baptist Publications.

TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO!

Tarehe 3-9 katika mwezi wa Machi ni Juma la Maombi la Wanawake Wabatisti wa Afrika ya Mashariki. Wakati ule ukiwadia mtaweza kuweka kitabu hicho na kusoma Masomo ya Juma la Maombi. Masomo ya Juma la Maombi yatatumwa katika Kitabu kingine kabla ya wakati wa Maombi.





## SHIDA ZA NYUMBANI: UASHERATI NA KUOA ZAIDI YA MKE MMOJA

Wimbo
Maombi
Maandiko Matakatifu:

---Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo, lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili. 1 Wakorintho 10:13

Wimbo
Kuita Majina
Shughuli
Masomo

UTANGULIZI:

Mpango wa Mungu kwa nyumba ni ile isemayo mume inampasa aoe mke mmoja na hao wawili inawapasa wawe mwili mmoja. Mpango wa Mungu ni kwamba mume na mwanamke walale pamoja mara tu baada ya kuoana. Mpango wa Mungu ni kwamba mume na mke walale wao wawili pekee. Hili ni jambo la maana kwamba Mungu aliitoa amri yake, "Usizini," kama amri moja ya zile kumi. (Kutoka 20:24).

Yesu aliendelea kuieleza ile amri. Alisema ya kwamba ni dhambi kwa mwanamume kumtazama mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake. (Soma Mathayo 5:27,28.)

Leo tutajifunza kuhusu uasherati au uzinzi na kuoa zaidi ya mke mmoja. Hizi